TAARIFA YA HISTORIA YA WILAYA YA KONGWA

UTANGULIZI:

Wilaya ya Kongwa ni miongoni mwa Wilaya sita za ambazo zinapatikana katika Mkoa wa Dodoma. Wilaya hii ipo kati ya Latitude 3^0 Kusini na 6.0^0 Kusini mwa Ikweta na Longitude 36.0^0 hadi 36.5^0 Mashariki mwa Greenwich. Mwinuko unafikia Mita 1200 kutoka usawa wa bahari.

Wilaya ya Kongwa inapakana na Wilaya ya Kiteto kwa upande wa Kaskazini; kwa upande wa Magharibi inapakana na Wilaya ya Chamwino; Mashariki inapakana na Wilaya ya Gairo; na upande wa Kusini inapakana na Wilaya ya Mpwapwa.

Wilaya hii ina ukubwa wa Kilometa za Mraba 4041. Kiutawala imegawanyika katika Tarafa 3, Kata 22, vijiji 75 na vitongoji 281. Wilaya ina jumla ya kaya 50877 zenye wakazi wapatao 309,973 wakiwemo wanaume 149,221 na wanawake 160,752. Takwimu hizi ziznazingatia ongezeko la watu la wastani wa 2.4% kwa mwaka kulingana na Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012.

Wenyeji wa Wilaya hii ni Wagogo, Wakaguru, na Warangi. Pia kuna makabila mengine ambayo yalihamia toka sehemu mbambali za Tanzania kama vile Wabena, Wanguu, Wakamba na Wamasai ambao walikuja kwa ajili ya shughuli za kilimo na mifugo.

Shughuli kuu za kiuchumu zinazofanywa na wakazi wa Wilaya ya Kongwa ni ufugaji wanyama (ng’ombe, mbuzi, kondoo, na punda). Punda hutumika zaidi katika usafirishaji wa mazao. Pia shughuli za kilimo cha mazao ya chakula na biashara mfano mahindi, mtama, uwele, karanga na alizeti.

HISTORIA YA WILAYA YA KONGWA

1. KUJULIKANA KWA KONGWA:

Wilaya ya Kongwa lianza kujulikana katika ramani ya Dunia mwaka 1913 ambapo Shirika la Kidini kutoka Canada ambalo lilijulikana kama Church Missionary Society walipoanza ujenzi wa Chuo cha Ualimu na Theolojia mwaka 1909 katika kijiji cha Mlanga. Lakini kutokana na Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, ujenzi huo ulichukua muda mrefu hivyo kukamilika mwaka 1927. Vifaa vilivyotumika katika kujengea Chuo hicho ni mawe na chokaa iliyochomwa.

Chuo kilifundisha taaluma ya Uchungaji (Theolojia), Ualimu na Uuguzi. Wanafunzi waliosoma katika Chuo hicho walitoka sehemu mbalimbali za Tanganyika na Kenya. Miongoni mwa wanafunzi wa kwanza waliosoma katika Chuo hicho ni Mzee Musa Fungo na Yohana Malecela.

(Jengo *la Chuo cha Theolojia cha Mtakatifu Filipo kilichojengwa mwaka 1927 – Mlanga Kongwa*)

Wakati wa vita ya Wakoloni baina ya Waingereza na Wajerumani mwaka 1914 – 1918, wanafunzi 12 walisoma katika Chuo hicho walikamatwa na Wajerumani na kupelekwa Zanzibar kuhifadhiwa na vita ilipoisha walirudishwa. Wakazi wengi walioishi katika eneo la Mlanga, wengi wao ni wahamiaji toka sehemu za Berege (Morogoro), Tanga na Iringa na Kiongozi wao kwa kipindi hicho alikuwa anaitwa Chifu Mahinyila. Katika eneo la Mlanga karibu na mlima kuna alama za miguu ya Farasi ambao walipitishwa katika njia hiyo na Wakoloni wakati wa vita.

Baada ya vita ya Kwanza ya Dunia baina ya Waingereza na Wajerumani Mlanga iliendelea kupanuka kutokana na shughuli za kilimo cha karanga na watu wengi kuja kuishi hapo ndipo mji uliposogea hadi Mnyakongo. Mwaka 1922 soko lilianzishwa katika eneo la Uhindini baada ya kuonekana kua hakuna soko na wananchi wengi walikuwa wanasafirisha mazao yao kwa umbali mrefu hadi Gulwa – Mpwapwa. Miongoni mwa Waafrika waliokuwa na duka katika soko hilo ni Mzee Musa Fungo.

Mwaka 1932, Punda weupe ambao walijulikana kama Maskati waleletwa ili kutumika katika kusafirisha mizigo pamoja na rising (wheel chair) ambayo yalitumiwa zaidi na wanawake tu katika usafiri.

Kongwa ilipata umaarufu baada ya vita Kuu ya Pili ya Dunia, ambapo Shirika moja la kilimo la Uingeraza lililojulikana kama Overseas Food Cooperation kuanzisha utafiti wa kilimo cha karanga mwaka 1947 katika eneo kilipo kituo cha Afya Ugogoni kwa madhumuni ya kufufua Uchumi wa Uingeraza uliokuwa umeathiriwa na Vita Kuu hiyo. Pia ilikuwa kuwapatia ajira Wanajeshi wa Kiingeraza walorudi toka vitani. Hatimaye baada ya utafiti huo mwaka 1948 kilimo cha karanga kilianzishwa rasmi katika wilaya ya Kongwa na watu wa baadhi ya nchi zilizotawaliwa na mwingereza mfano India, Somalia ma Mauritius walikuja kuishi ns kuendesha kilimo cha karanga. Maeneo mbalimbali yalifyekwa ili kuandaa mashamba kuanzia Kongwa, Zoissa hadi Sagara. Kwa wakati huo mashamba yalimilikiwa na Wazungu wenyewe na Waafrika walikuwa ni vibarua katika mashamba ambapo Wamauritius waliofanya kazi za udereva na Ufundi katika mashamba hayo. Kuwepo kwa Wamauritius katika eneo la Kongwa kulipelekea kuanzishwa kwa eneo lililojulikana kama Morisheni ambalo lilitokana na watu wa Kongwa kutamka Wamauritius ndipo walipoamua kutohoa na kuitwa Morisheni. Eneo hili pia lilitumiwa na wapigania uhuru kama sehemu ya makaburi, kuzika wale waliofariki kwa sababu mbalimbali.

Picha:

(Baadhi ya makaburi ya wapigania Uhuru wa Msumbiji, Namibia na Afrika Kusini.)

2. CHIMBUKO LA WILAYA YA KONGWA NA MAENDELEO KATIKA SEKTA ELIMU, AFYA NA MIUNDO MBINU:

Kutokana na kuanzishwa kwa kilimo cha karanga na Shirika la Uingeraza, Overseas Food Cooperation (OFC) katika Kongwa, kilimo hicho kilipelekea kuongezeka kwa shughuli nyingi za Utawala na biashara zilizofuatana na kuwepo kwa Shirika hilo na Kongwa ilipata hadhi ya kuwa Wilaya kamili mnamo mwaka 1950.

Aidha kilimo cha karanga kilipelekea ujenzi wa shule ya Mnyakongo mwaka 1948 hadi 1949 amabayo iliojulikana kama European School na ilikuwa na Darasa la I hadi Kidato cha VI na waliosoma shule hiyo ni watoto wa kizungu tu, wakati Waafrika walisoma katika shule iliojulikana kama Bush School na baada ya kuhitimu masomo yao walipelekwa kuendelea na masomo katika chuo cha St. Philips. Sambamba na shule, walijenga pia Hospitali mwaka 1948 hadi 1949 ambayo ilitegemewa na wakazi wa Afrika Mashariki kwani ilikuwa na Madaktari bingwa na Chuo cha Afya kilikuwepo katika Hospitali hiyo. Mwaka 1951 hadi 1952 walijenga

Gereza la Kongwa na reli iliyoanzia Msagali – Kongwa – Songambele amabayo ilijengwa mwaka 1947.

Picha:

(*Jengo la Stesheni ya reli ya Kongwa – Songambele, lilijengwa mwaka 1949*)

Majengo yalijengwa na Mwingereza aliyeitwa Landar. Miaka miwili baadaye wilaya hii ilifutwa kutokana na kushindwa kwa mradi wa kilimo cha karanga ambao ulisababishwa na ukosefu wa mvua kwa miaka mitatu mfululizo na shirika la OFC kufunga shughuli zake na Kongwa kurudishwa kuwa wilaya ndogo chini ya Wilaya ya Mpwapwa.

3. **KUANZISHWA KWA SHIRIKA LA NARCO:**

Baada ya kushindwa kwa mradi wa karanga Ndugu Clenton ambaye alikuwa ni Kaburu na aliyefahamika kama Mwamba na Waafrika alianzisha ufugaji wa ng'ombe katika Ranchi ya Tanganyika Agriculture Corporation ambayo kwa sasa ni NARCO.

4. **KONGWA KATIKA HARAKATI ZA KUPIGANIA UHURU:**

Mnamo February 1955 Chama cha TANU kilifangua tawi la Chama hicho katika Wilaya ya Kongwa na kumchagua Mzee Tito Fungo kuwa Mwenyekiti I wa Chama katika Wilaya. Baada ya kuchaguliwa Mzee Tito Fungo alianza kuendesha mikutano katika sehemu za Mlali, Sagara, Songambele, Njoge na maeneo mengine ili kuhamasisha wananchi kujiunga na Chama cha TANU na kufungua matawi madogo katika sehemu hizo. Kutokana na jitihada zake kuwahamasisha wananchi kujiunga na TANU ili kusaidia kuleta ukombozi, Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa ambaye alikuwa Mtawala wa kikoloni akliamua kwa makusudi kumteua Mzee Tito Fungo kuwa Mshauri Mjuzi wa Halmashauri ya Mpwapwa mwaka 1958 nia ni kumfunga mdomo aache kuhamasisha wananchi kuhusu Uhuru. Katika kipindi cha kudai uhuru Mwenyekiti wa TANU Mzee Tito Fungo aliwahamasisha wananchi kuchangia fedha ili kununua gari ambalo litasaidia kuendesha shughuli za Chama na walifanikiwa kununua gari aina ya Land Rover kwa Tshs. 16,000/-. Katika kipindi cha mwaka 1958 hadi 1960 Hayati Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere amabaye alikuwa Mwenyekiti wa TANU taifa alifika Kongwa na kufanya mikutano ya kuwahamasisha wananchi kudai Uhuru wa nchi yao.

5. **SHAMRASHAMRA ZA UHURU:**

Mwaka 1961 wakati Tanganyika inapata Uhuru, katika Wilaya ya Kongwa wananchi waliamua kufanya kikao na kuunda kamati ya sherehe chini ya Mwenyekiti wao Jobu fun go ambaye aliwataka wananchi kujadili namna wtakavyosherekea siku ya uhuru. Walikubaliana kujenga mnara ambao utatumika kupandisha Bendera ya Uhuru wa Tanganyika na aliyejitolea kujenga mnara alikuwa ni Mzee Sadru Remtullah. Aidha, Meshack Magabo na wananchi wengine walijitolea kwenda kwuwasha moto katika mlima wa Sang'anga huku wengine wakirusha mafataki katika maeneo mbalimbali ya Kongwa.

Picha:

(*Mnara uliojengwa na Mzee Sadru Remtullah ambapo bendera ya Uhuru ilipandishwa mwaka 1961*)

Mara baada ya uhuru wananchi wengi walijitokeza zaidi katika kufanya kazi kutokana na kuitikia wito wa Mwl. Nyerere kuwa Uhuru Ni Kazi. Katika kuwahimiza wananchi kufanya kazi kwa bidii Mwl. Nyerere alikuja Kongwa katika kijiji cha Ndungurumi, Songambele, na Mseta ili kuhamasisha kilimo cha bega kwa bega na kisomo cha manufaa mwaka 1975 hadi 1976.

6. KUJENGWA KWA KAMBI YA WAPIGANIA UHURU:

Kuwepo kwa wapigania Uhuru Wilaya ya Kongwa kunafuatia ziara ya Marehemu Oscar Kambona aliyekuwa Waziri wa mambo ya nje, Waziri wa ulinzi, Katibu Mkuu wa TANU mwaka 1963, Machi ambapo alifanya mkutano wa hadhara katika jengola TANU Kongwa na kuwaambia wananchi kwamba Waafrika wenzetu wa nchi za Msumbiji, Namibia, Afrika ya Kusini, Zimbabwe na Angola wanateswa na wa nahitaji kupata Uhuru. Na Uhuru wao wataupata kwa mtutu wa bunduki, hivyo watakuja Tanzania – Kongwa kujifunza mbinu za kuwang'oa wadhalimu waliokuwa wanatawala nchi zao hivyo wapewe msaada, ushirikiano wa hali na mali.

Mnamo mwaka 1964 shughuli za kuwapokea wapigania Uhuru katika Wilaya ndogo ya Kongwa zilianza na kutanguliwa na wapigania Uhuru wa vyama vya Frelimo (Msumbiji), MPLA (Angola), SWAP (Namibia), PAC na ANC (Afrika ya Kusini), ZANU PF (Zimbabwe).

Tofauti ya ujio wao ilikuwa ni miezi tu, lakini, wote walifika ndani ya mwaka huo 1964. Kwa kuwa mchakato wa ukombozi wa nchi hizo ulikuwa unasimamiwa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika – OAU, Tanzania ilikuwa kituo cha kuwahifadhi wapigania Uhuru. OAU ilimteua Ndugu B.M. Kibasa amabaye alikuwa ni Mtanzania kuwa Civilian Administrator katika kuongoza shughuli zote za wapigania Uhuru, wakiwemo Watanzania wafuatao; Major Yusuph Mohamed Chongambele, Col. Isack Mwisongo, Lt. Maganga pamoja ns wengine kutoka nchi mbalimbali ulimwenguni.

Katika kuzingatia historia ya wapigania Uhuru, hasa Namibia wafuatao wanakumbukwa na wananchi wa Kongwa; Sam Nujoma – Raisi wa kwanza Namibia, David Ushona – mdogo wake Sam Nujoma na Sofia Ushona – binti wa David Ushona.
Picha:

(*Moja ya madarasa yaliyotumiwa na Wapigania Uhuru kwa ajili ya mafunzo ya kijeshi*)

Picha:

(*Jengo la Utawala lililotumiwa na wapigania Uhuru wa Kusini mwa Afrika 1964*)

Picha:

(*Jengo la bweni lililotumiwa na wapigania Uhuru wa Kusini mwa Afrika.*)

7. UHUSIANO KATI YA WANANCHI NA WAPIGANIA UHURU WA CHAMA CHA SWAPO:

Kwa kipindi chote ambacho wapigania Uhuru walipokuwa wakiishi Wilayani Kongwa, mahusiano baina ya wananchi na wapigania Uhuru, hasa kwa Wanamibia yalikuwa ni mazuri sana. Ulikuwapo ushirikiano mkubwa sana kati yao na wananchi, walikuwa wasikivu, watulivu, walishirikiana na wananchi katika shughuli mbalimbali zikiwemo maadhimisho ya siku mbalimbali za Kitaifa; Mfano "Saba Saba", Uhuru na Jamhuri, Muungano, Mei Mosi n.k.
Pia walioshiriki kucheza michezo mbalimbali pamoja na wananchi ikiwemo mipira ya pete na Mpira w miguu. Kadhalika walishirikiana na wananchi katika shughuli za maendeleo mfano; ujenzi wa Jumba la Maendeleo Kongwa amabalo lilijengwa mwaka 1967.

Pale walipohitaji msaada toka kwa wananchi walipewa, kwa mfano kujifunza lugha ya Kiswahili – Mwl. Hilda Malogo alishiriki kikamilifu kuwafundisha lugha ya Kiswahili. Wanafunzi waliofundishwa na Mwl. Hilda Malogo ni pamoja na Sam Nujoma, David Ushona, Limo, Hayati Samora Machel aliyekuwa Rais wa Msumbiji. Walijifunza pia na lugha ya Kigogo.

Wananchi wa Kongwa walipata shughuli ya kusambaza vyakula kwa wapigania Uhuru wa Namibia, hivyo walipata kipato kutokana na mahusiano mazuri yaliyokuwapo kati yao. Wapigania Uhuru waliweza kuwaoa binti za wananchi wa Kongwa na baadhi yao waliondoka nao hadi Namibia, hivyo kuendeleza udugu wa damu.

Kwa ujumla, wapigania Uhuru wote walikuwa na Imani kubwa sana kwa Chama cha TANU na Serikali yake, kwani lengo lilikuwa ni kupatikana kwa Uhuru katika nchi hizo kwa nayakati tofauti.

8. **KUJENGWA KWA HANDAKI LA KIHISTORIA KONGWA:**

Mnamo mwaka 1968 wapigania Uhuru walikuwepo katika Wilaya ya Kongwa walijenga Handaki amabalo lilitumiwa na Rais wa kwanza wa Msumbiji Hayati Samora Machel kama Ofisi yake. Handaki hilo lilijengwa na Mzee Mabaya amabaye alikuwa ni raia wa Afrika Kusini na lilikuwa na urefu wa Mita 150 na kina kipatacho Mita 4. Pamoja na uwepo wa kambi ya wapigania Uhuru na Handaki, Kusini mwa eneo hilo kulikuwapo pia Gofu la Kanisa amabalo Waingereza walisali humo wakati wa kampuni ya OFC mwaka 1974. Gofu hilo la Kanisa lipo katika Kitongoji cha Mnyakongo na lilitumiwa na dhehebu la Anglikana.

Picha:
(Handaki *lililotumiwa na Rais wa Msumbiji, Hayati Samora Machel*)

Picha:

(*Gofu la Jengo ambalo lilikuwa Kanisa la Kianglikana lililotumiwa na Waingereza*)

9. **KUUNDWA KWA HALMASHAURI YA KONGWA:**

Baada ya nchi nyingi zilizo Kusini mwa Afrika kupata Uhuru kwenye miaka ya **1970 – 1990**, kambi ya wapigania Uhuru wa Kusini mwa Afrika ilianza kutumika na Jeshi kama kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (**JWTZ**) hadi **Agosti, 1994**. Miongoni mwa viongozi wa Jeshi hilo ambao waliwahi kuishi Kongwa ni Mkuu wa Majeshi **Davis Mwamunyange**.

Mwaka **1995** kambi ya wapigania Uhuru ya Kongwa ilifungwa rasmi na majengo yake yalikabidhiwa kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni na kuanzishwa kwa shule ya kutwa ya **Sekondari Kongwa**. Baadhi ya wapigania Uhuru ambao walibaki kabla ya kufungwa kwa kambi walichukuliwa na kuhamishiwa katika kambi ya wakimbizi iliyopo eneo la **Mazimbu Mkoani Morogoro**.

Kwa kipindi chote cha wapigania Uhuru hadi kufungwa kwa kambi, Kongwa ilikuwa ni Wilaya ndogo chini ya Wilaya ya Mpwapwa. Na tarehe **23 Juni, 1995** Serikali ilitoa tangazo la Serikali kuipatia hadhi Kongwa kuwa Wilaya kamili kwa mara nyingine kwenye kikao cha Bunge mjini Dodoma. Mipaka yake ilitangazwa kwenye gazeti la Serikali la tarehe **8 Novemba, 1996** (**Tangazo la Serikali Na. 349**)

Tarehe **23 Oktoba, 1995** Mkuu wa kwanza wa Wilaya aliteuliwa na kuapishwa mjini Dodoma tarehe **21 Novemba, 1995** na kuanza kazi tarehe **22 Novemba, 1995**. Baada ya mabadiriko hayo, miaka **9** baadaye **Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa** iliundwa na kuanza kazi rasmi tarehe **23 Julai, 2004**.

Miongoni mwa viongozi walioongoza Wilaya hii hadi kufikia sasa ni kama inavyoonekana katika majedwali hapo chini.

Jedwali Na 1. WAKUU WA WILAYA (DCs)

Na.	Majina	Mwaka Alioingia	Mwaka Aliotoka
1.	MHE. LEPILAH OLE MOLOIMET	1995	1999
2.	MHE. PENIEL OLE SITABAU	1999	2003
3.	MHE. FLORENCE A. HOROMBE	2003	2006
4.	MHE. LEMBRIS M. KIPUYO	2006	
5.			
6.			

Jedwali Na 2. WENYEVITI WA HALMASHAURI (CCPs)

Na.	Majina	Mwaka Alioingia	Mwaka Aliotoka
1.	MHE. RICHARD NJALIKA	1995	2000
2.	MHE. HAYATI WILLIAM SHITINDI	2000	2010
3.	MHE. WHITE ZUBERI MWANZALILA	2011	Hadi sasa

Jedwali Na 3. WAKURUGENZI WATENDAJI (DEDs)

Na.	Majina	Mwaka Alioingia	Mwaka Aliotoka
1.	TITUS LEMUNGE	1996	1997
2.	MPANGALOKELA TATARA	1998	2000
3.	THABITA I. MSHAKANGOTO	2000	2003
4.	JIMMY K. MLAY	2003	2006
5.	JACKSON H. SAMWELI	2006	2008
6.	ATHUMAN O. AKALAMA	2008	2010
7.	BIBIE MNYAMAGOLA	2010	Hadi sasa

Jedwali Na 4. WABUNGE (MPs)

Na.	Majina	Mwaka Alioingia	Mwaka Aliotoka
1.	MHE. GIDION SENYAGWA	1975	2000
2.	MHE. JOB Y. NDUGAI	2000	Hadi sasa

10. **MUUNDO WA WILAYA YA KONGWA:**
Wilaya ya Kongwa ina muunganiko wa pande mbili; **Serikali Kuu** na **Halmashauri ya Wilaya**.

1: **Serikali Kuu**
Kwa upande wa Serikali Kuu imegawanyika kama ifuatavyo:-

i. Mkuu wa Wilaya (**DC**)
ii. Katibu Tawala wa Wilaya (**DAS**)
iii. Afisa Usalama wa Wilaya
iv. Afisa Magereza wa Wilaya
v. Mkuu wa Polisi wa Wilaya
vi. Hakimu Mfawidhi wa Wilaya
vii. Meneja TRA.

2: Halmashauri ya Wilaya
Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ina muundo sawa na zilivyo Halmashauri zingine zote nchini Tanzania.
Halmashauri hii imeundwa na Baraza la Madiwani na Timu ya Wataalamu inayoongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya. Kwa hivi sasa Halmashauri ina Kamati za kudumu 6 ambazo ni; **Kamati ya Fedha; Kamati ya Utawala na Mipango; Kamati ya Elimu, Afya na Maji; Kamati ya Ujenzi, Mazingira, na Uchumi; Kamati ya Ukimwi; Kamati ya Maadili; na Kamati ya Huduma za Jamii**.

Kwa upande wa Idara, Halmashauri ina Idara **10** na Vitengo **6** ambavyo ni; **Kitengo cha Sheria; Kitengo cha Manunuzi; Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani; Kitengo cha TEHAMA; Kitengo cha Nyuki; na Kitengo cha Biashara.**

Idara za Halmashauri ni:-

i. Idara ya Utumishi
ii. Idara ya Fedha
iii. Idara ya Ujenzi
iv. Idara ya Elimu Msingi
v. Idara ya Elimu Sekondari
vi. Idara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira
vii. Idara ya Kilimo, Mifugo na Ushirika
viii. Idara ya Maendeleo ya Jamii
ix. Idara ya Mipango
x. **Idara ya Afya**.

11. **VIONGOZI WA KUCHAGULIWA:**
Halmashauri ina viongozi wa siasa – wa kuchaguliwa ambao ni:-

i. Mbunge Jimbo la Kongwa
ii. Mwenyekiti wa Halmashauri
iii. Madiwani wa kuchaguliwa 22 (hawa ni pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri)
iv. Madiwani viti maalum – wanawake 7

Tanbihi:-

Kwa sasa Madiwani wa viti maalum wote waliopo wanatoka CCM.
Katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii, Wilaya majukumu na malengo yafuatayo:-

a. Kutoa huduma bora kwa jamii
b. Kuhakikisha kuwa ulinzi na usalama unaimarishwa miongoni mwa wananchi
c. Kuhakikisha kwamba Utawala bora na Uzingatiaji wa haki za binadamu unafuatwa katika Wilaya
d. Kuimarisha shughuli mbalimbali za kiutamaduni na kijamii.

12. **MAENDELEO:**

Mabadiliko na Matukio Makuu yalitokea katika mfumo wa kisiasa, kiulinzi, Kiutawala, kiteknolojia, kiuchumu na kijamii katika Wilaya ya Kongwa tangu mwaka **1961** hadi sasa. Mabadiriko hayo ni:-

(i) **KISIASA:**

Mara baada ya Uhuru **1961**, maeneo mbalimbali ya Tanzania Kongwa ikiwa mojawapo yalikuwa na mfumo wa Chama kimoja cha siasa kinachotawala ambapo hapo mwanzo kulikuwa ni **TANU** na baadaye **1977 CCM**. Lakini ilipofika mwaka **1992** mfumo wa vyama vyingi ulianza rasmi ambapo katika Wilaya ya Kongwa kuna vya vya siasa vipatavyo **6** – ambavyo ni **CCM, CHADEMA, CUF, TLP, UDP, na NCCR – MAGEUZI**. Kwa kipindi chote hicho Chama kilichofanikiwa kuongoza Wilayani Kongwa ni Chama cha Mapinduzi – **CCM**.

(ii) **KIULINZI:**

Hapo awali, shughuli za ulinzi katika Wilaya ya Kongwa ilikuwa ni jukumu la Polisi tu, lakini baadaye, katika miaka ya **1990** na **1991** suala la ulinzi lilikuwa ni la kijamii nzima ambapo kilianzishwa **sungu-sungu** (watu walikuwa wanafanya ulinzi kwa zamu katika maeneo yao).

Aidha kaitika kufanikisha ulinzi wananchi waliandaliwa ipasavyo katika shughuli za ulinzi kwa kushiriki kikamilifu katika mafunzo ya Jeshi la **Mgambo** na **JKT**.

(iii) **KIUTAWALA:**

Kiutawa, Kongwa kabla ya Uhuru ilikuwa chini ya **Watemi** na **Machifu** wa makabila ambao ndiyo walikuwa wanatawala katika maeneo mbalimbali kwa kurithishana.
Mfano:-

- Mtemi Nyamwanji – alitawala Pandambili
- Mtemi Mahinyila – alitawala Kongwa
- Mtemi Kasawa – alitawala Mlali
- Mtemi Simango – alitawala Sagara.

Mara baada ya Uhuru, Mfumo wa Utawala ulibadirika kutoka ule wa **kurithishana** na kwenda mfumo wa **kidemokrasia** ambapo jamii husika ilipata nafasi ya kumchagua Kiongozi wamtakaye, mfano wenyeviti wa vijiji, vitongoji, balozi wa nyumba kumi, n.k.

(iv) **KITEKNOLOJIA:**

Hapo awali shughuli nyingi hazikuwa katika mfumo wa kiteknolojia. Kwa mfano, utunzaji wa nyaraka mbalimbali za kumbukumbu zilihifadhiwa katika majalada lakini kwa sasa zinahifadhiwa katika Ngamizi (**Computer**) – kuna mifumo ya Ngamizi (**Computer Database Systems**) kama **HCMIS**, **IFMIS**, **PlanRep**, n.k. kwa kufuata mabadiriko ya kiteknolojia yaliyojitokeza katika ufanisi wa kazi mbalimbali. Pia, baadhi ya taarifa huhifadhiwa katika database ya tovuti ya Wilaya ya Kongwa inayoendelezwa na Mtaalamu wa Halmashauri (**Afisa TEHAMA**).

Mawasiliano mengi wakati Wilaya inaanza yalifanyika kwa njia ya barua, telegram ambapo kwa sasa yanafanyika kwa njia ya simu za mkononi, barua pepe (**Email**), barua nukushi (**Fax**), na kwenye vyombo vya habari kama vile redio, magazeti pamoja na runinga (**TV**).

Kwa upande wa usafiri hapo mwanzo watu walikuwa wanatembea kwa miguu umbali mrefu, walitumia wanyama mfano punda na farasi lakini baada ya mabadiriko ya kiteknolojia sasa kuna vyombo vya usafiri vingi katika maeneo mbalimbali ya Kongwa mfano mabasi, pikipiki na baiskeli.

Kabla ya Uhuru watu wa Kongwa walilima kwa kutumia jembe la mkono, nafaka zilisagwa kwa kutuia mawe, kukobolewa kwenye kinu lakini teknolojia imebadirika na watu wanatumia mashine ya kusaga nafaka na kulima wanatumia trekta.

Kwa upande wa nishati, kabla ya Uhuru wakazi wengi walitumia nishati iliyotokana na kuni na mara baada ya Uhuru nishati ya mkaa ilianza kutumika, majiko ya umeme, ya mafuta, yanayotumia pumba za mahindi pamoja na mavumbi ya mbao (**Saw dust**) yanatumika pia.

Katika ufugaji wa wanyama kama vile ng’ombe, mbuzi na kondoo njia za asili zilitumika lakini kutokana na mabadiriko ya kiteknolojia baadhi ya wafugaji wanapata mafunzo ya kuanza kutumia njia za kisasa katika ufugaji, mfano upandikizashaji (**Artificial Insemination**).

Mbali na hayo katika mabadiriko ya kiteknolojia katika sekta ya Afya, kabla ya Uhuru jamii nyingi Wilayani Kongwa zilitumika dawa za asili. Lakini mara baada ya Uhuru hadi sasa huduma za afya zinapatikana katika **Hospitali**, **Zahanati** na **Vituo vya Afya**.

(v) **KIUCHUMU:**

Katika shughuli za kiuchumu katika Wilaya ya Kongwa kabla ya Uhuru katika Kilimo na Mifugo, jamii nyingi zilikuwa zinatumia nafaka na kwa kufuga wanyama kwa ajili ya chakula lakini kwa sasa shughuli hizo zinafanyika Kibiashara zaidi.

Kabla ya Uhuru hakukuwa na Asasi za kifedha za kuwawezesha wananchi kuipatia mitaji kwa ajili aya uanzishaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumu. Lakini baada ya Uhuru Asasi nyingi za Fedha zilianzishwa kwa lengo la kuwawezesha wananchi, mfano; national microfinance bank (**NMB**), **Benki ya Posta**, **Finca**, **SIDO**, **Tunakopesha Ltd**, **Mfuko wa Rais wa Kujitegemea**, vyama vya kuweka na kukopa (**SACCOS**) – mfano **KODSACCOS**, **KOTESACCOS** na **VICCOBA** (vikundi vya kijamii vya kuweka na kukopa).

(vi) **KIJAMII:**

Katika Wilaya ya Kongwa, Makazi ya jamii nyingi kabla ya Uhuru yalikuwa ya nyumba za udongo zilizoezekwa kwa kutumia nyasi (**Tembe**) na mara baada ya Uhuru jamii nyingi zilianza kujenga nyumba bora na za kisasa zaidi zilizoezekwa kwa kutumia mabatia na vigae.

Kwa upande wa dini, kabla ya Uhuru hakukuwa na madhehebu mbalimbali ya Kidini katika Wilaya ya Kongwa. Lakini baada ya Uhuru madhehebu mengi yalianzishwa ambayo yamekuwa na mchango mkubwa katika kuleta ufanisi wa maendeleo ya huduma za kiroho na kimwili kwa mfano:-

- Kanisa Katoliki (**RC**) – Kwa ujumla linamiliki shule mbili za sekondari (St. Francisco na St. Pio), Kituo cha kulelea watoto wenye ulemavu Mlali, Zahanati 1 iliyopo katika Parokia ya Kongwa na Shule ya Awali.
- K.K.K.T. – Wanamiliki shule ya awali na kituo cha kulelea watoto waishio katika mazingira hatarishi **(Compassion**).
- Anglikana – Wanamiliki shule ya awali 1 na Vituo 4 vya kulelea watoto waishio katika mazingira hatarishi – Matongoro, Songambele, Mtanana na kongwa.
- E.A.G.T. – Inamiliki Shule ya Awali 1 na Kituo 1 cha kulelea watoto waishio katika mazingira hatarishi.
- Bakwata – Inamiliki Shule ya Awali 1.
- Kanisa la Sabato – Linamiliki Zahanati 1 iliyopo Mkoka.

Sambamba na hilo, kabla ya Uhuru Wilayani Kongwa hakukuwa na Asasi zisizo za Serikali (**NGOs**) ambazo zinatoa huduma mbalimbali ya kijamii. Lakini baada ya Uhuru hadi sasa mabadiriko mbalimbali ya kijamii yametokea kwani sasa kuna Asasi zisizo za kiserikali zilizoanzishwa Wilayani ambapo zinatoa huduma za kijamii mfano:-